**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

***Dar es Salaam***
***04 Februari, 2025***

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amepokea Tuzo Maalum ya Kimataifa ya Global Goalkeeper Award kutoka kwa taasisi ya Gates Foundation.

Tuzo hiyo imetolewa katika hafla maalum iliyofanyika katika Hoteli ya Hyatt Regency kwa kutambua jitihada za makusudi zilizofanywa kwenye sekta ya afya na mafanikio ya Serikali ya Tanzania katika kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto wachanga chini ya umri wa miaka mitano.

Tuzo hiyo ambayo hutolewa kwa viongozi waliowezesha nchi zao kuharakisha maendeleo kuelekea kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals – SDGs) imekabidhiwa kwa Rais Dkt. Samia na Dkt. Anita Zaidi, Rais wa Kitengo cha Usawa wa Jinsia kutoka Taasisi ya Gates.

Akizungumzia tuzo hiyo, Rais Dkt. Samia amesema kuwa kati ya mwaka 2020 hadi 2024 uwekezaji uliofanywa na Serikali kwenye sekta ya afya imewezesha Tanzania kuongeza vituo vya kutolea huduma za afya vinavyotoa huduma za dharura za mama na mtoto kutoka 340 hadi 523.

Aidha, wataalam wabobezi wa kiafya wa masuala ya mama na mtoto kutoka 69 hadi 338, na kuongeza mashine za ***ultrasound*** na ***sonograph*** kutoka 345 hadi 970.

Rais Dkt. Samia amesisitiza kuwa Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika kuimarisha lishe ili kutokomeza utapiamlo na udumavu kwa watoto nchini.

Rais Dkt. Samia amesema kuwa ameipokea tuzo hiyo kwa heshima ya watumishi wote katika sekta afya ambao kujitoa kwao, ujuzi na ustahimilivu wao umewezesha nchi kufanya maendeleo kwenye sekta hiyo.

Sharifa B. Nyanga
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu